# Orodha ya stadi: Namna ya kuchagua mtumiaji wa vifaa saidizi vya kuhama anayestahili

TAP

| Mshiriki wa Mafunzo: | Mwezeshaji: | Tarehe: |
|---|---|---|

| Sifa | Maelezo ya Mwezeshaji | Ndio | Hapana |
|---|---|---|---|
| **Uchunguzi kabla ya kugawa vifaa saidizi** | | | |
| 1. Inaelezea uchunguzi:<br>• Inaanisha kile ambacho uchunguzi unahusu<br>• Inatoa fursa ya kuuliza maswali<br>• Uliza kama mgonjjwa anatoa ridhaa<br>2. Osha mikono | | | |
| **Kipimo rahisi cha kusogea kutoka eneo moja hadi jingine na kipimo cha kihatarishi cha kiafya.** | | | |
| 3. Uliza kama maswali yanayohusu uwezo wa kusogea kutoka eneo moja hadi jingine na kihatarishi cha kiafya:<br>• Ainisha vihatarishi kwa kadri mgonjwa anavyotoa majibu<br>• Amua kwa usahihi kama kuna umuhimu wa kukamilisha vizuri uchunguzi wa mguu (Sehemu ya 3) | | | |
| **Uchunguzi wa sehemu ya kutembelea ya mguu** | | | |
| 4. Fanya kwa usahihi kipimo cha sehemu ya kutembelea ya mguu<br>• Maswali na mambo yanayoweza kuonekana.<br>• Kipimo cha mapigo ya moyo<br>• Kipimo cha muda wa kujazia damu kwenye kiungo<br>• Kipimo cha hisia | | | |
| 5. Toa kwa usahihi muhtasari wa kihatarishi cha kidonda cha sehemu ya kutembelea ya mguu | | | |
| **Chagua kifaa saidizi na huduma nyingine.** | | | |
| 6. Tumia maswali ya kuchunguza ili kutambua kama mgonjwa anaweza kufaidika na vifaa saidizi vya kusogea na huduma nyinginezo. | | | |
| **Weka mpango** | | | |
| 7. Tengeneza mpango mzuri:<br>• Unahusu mtu anayepanga | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • Unaonyesha kama kuna uchunguzi na/au tathmini inayohitajika.<br>• Unahusu kumfundisha mtu ambaye yuko kwenye hatari ya kupata maambukizi kwenye mguu juu ya utunzaji wa mguu na kuhusu uvaaji wa viatu vizuri.<br>• Toa rufaa muafaka.<br>• Weka tarehe ya ufuatiliaji (kama itatakiwa) | | | |

## Mambo ya kuzingatiwa na Mwezeshaji

**Tumia Orodha hii ya Stadi kukusaidia:**

- Tathmini namna Washiriki wa Mafunzo wanavyotekeleza stadi za za kifaa saidizi cha kutembelea na kama Tathmini namna Washiriki wa Mafunzo wanavyotekeleza stadi za za kugawa kifaa saidizi cha kutembelea na kama
    - Wanaweza kufanya uchaguzi wa kifaa saidizi cha kutembelea bila kupewa msaada kutoka kwa mtu mwingine, au
    - Wanahitaji mafunzo zaidi ya vitendo na kama ndicho hicho wanachokihitaji, tambua aina ya stadi wanazohitaji kufanyia mazoezi

**Kumbuka kuwa:**

- Hii Orodha ina Stadi muhimu ambazo ziko kwenye moduli ya TAP.
- Inawezekana kuna stadi nyingine ambazo ungependa Watoa huduma wako kuwa nazo. Unaweza kuziongeza kwenye Orodha hii kama kwa kufanya hivyo itasaidia zaidi.

**Ili kutumia Orodha ya Stadi:**

- Fuatilia kwa karibu namna ambavyo Washiriki wa Mafunzo wanagawa vifaa saidizi vya kutembea. Hii naweza kufanyika kwa kufanya igizo (mmoja akiwa Mteja mwingine kama Mtoa huduma) au kufanya igizo na Wateja.
- Kila mara hakikisha kuwa mazoezi na wateja yanafanyika kwa usalama.
- Andika kwenye fomu kama Mshiriki wa Mafunzo amefanya kila stadi kwa usahihi. Andika maelezo kwenye eneo la kutoa maoni. Hii inaweza kuwa vitu ambavyo Mshiriki wa Mafunzo amefanya vizuri zaidi au maeneo ambayo anapaswa kuboreshwa zaidi/anahitaji mafunzo zaidi

**Utoaji wa mrejesho kwa Washiriki wa Mafunzo**

- Jadili na Washiriki wa Mafunzo kuhusu mambo uliyoyaona. Wajulishe mambo wanayoyafanya vizuri na maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.
- Wape nakala ya Orodha ya Stadi iliyokamilika kwa ajili ya wao kuweka kumbukumbu.
- Endelea kutoa mafunzo kwa vitendo na msaada pale unapohitajika na fanya tathmini mara nyingine ili kuboresha stadi zao na kujenga hali ya kujiamini.

- **Ni wakati gani Mshiriki wa Mafunzo anaweza kugawa vifaa saidizi vya kutembelea bila ya kupata usaidizi?**
- Ili kugawa vifaa saidizi vya kutembeleakwa usalama zaidi,mshiriki wa mafunzo anapaswa kukamilisha stadi zote kwa usahihi.
- Kumbuka- kutoa mafunzo kwa vitendo na kusimamia ni mchakato endelevu ili kuboresha stadi.